



Ripoti ya Kihaidrolojia

Ya Kila Mwezi (JNHPP)


Aprili (2026)

Muhtasari wa Hali ya Maji

Bwawa la Julius Nyerere Hydropower Plant (JNHPP) hupokea maji kutoka mito mikuu mitatu: Great Ruaha, Kilombero na Luwegu, ambayo ni sehemu ya Bonde la Rufiji. Mito hii ni muhimu kwa uzalishaji wa umeme wa maji, kilimo, matumizi ya majumbani na ikolojia.

Katika mwezi Aprili 2026, viwango vya maji vilikuwa juu ya wastani kwa asilimia 217 ikilinganishwa na wastani wa muda mrefu wa mwezi husika. Hali hii ilisababishwa na mvua kubwa katika vidakio pamoja na usimamizi endelevu wa rasilimali za maji. Aidha, usawa wa maji katika bwawa la JNHPP uliendelea kuimarika na kufikia kiwango cha juu cha uzalishaji wa umeme (184masl).

Zoezi la kupunguza maji kutoka katika bwawa la Julius Nyerere lilianza rasmi tarehe 15 Aprili 2026 na linaendelea. Mpaka kufikia tarehe 30 Aprili 2026 jumla ya mita za ujazo bilioni 4.6 zimepunguzwa kutoka katika bwawa ili kulinda usalama wa miundombinu ya bwawa.



Hali ya Hewa


Hali ya Mvua – Aprili 2026:

Takwimu za mvua zilizorekodiwa na vituo vya hali ya hewa katika maeneo mengi ya Bonde la Rufiji zilikuwa za wastani hadi juu ya wastani, na hivyo kuongeza mtiririko wa maji katika mito.

Mwelekeo – Mei 2026:

Kwa mujibu wa utabiri wa hali ya hewa uliotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA):

- Mvua zitaendelea kunyesha katika wiki ya kwanza na ya pili katika maeneo mengi ya bonde. Hata hivyo, mvua hizi zitakuwa ni kubwa zaidi katika mabonde madogo ya Kilombero, Luwegu na Lower Rufiji kuliko itakavyokuwa upande wa Great Ruaha.
- Wiki ya tatu na ya nne maeneo mengi ya bonde yatapokea mvua chache.



Hali ya Mtiririko wa Maji



Katika mwezi Aprili 2026, mtiririko wa maji uliendelea kuwa juu ya wastani kutokana na mvua zilizokuwa zinaendelea kunyesha katika maeneo mengi kwenye bonde.

Jedwali 1: Wastani wa Mitiririko wa Maji Mwezi (Aprili 2026) Ukilinganisha na LTA (2000–2025).

No.	Namba ya Kituo	Mto	Wastani i Mitiririko Aprili 2026 (m ³ /s)	Wastani Mitiririko LTA Aprili 2000–2025 (m ³ /s)	Maelezo
1	1KA3B	Great Ruaha at Msolwa	657	190	Juu zaidi ya wastani
2	1KB17	Kilombero at Swero	2488	1317	Juu zaidi ya wastani
3	1K3C	Luwegu at Mbarang'andu	520	450	Wastani

Uchambuzi wa Kihidrolojia


Wingi wa maji mitoni katika Mwezi Aprili 2026 umeongezeka. Hali hiyo imepelekea bwawa la Julius Nyerere kufikia kiwango cha juu cha uzalishaji cha 184masl. Hali hii imepelekea upunguzaji wa maji kuchukua muda wa takribani siku 16 mpaka kufikia mwisho wa mwezi wa Aprili 2026.



Viwango vya Maji Bwawani

Hali ya usawa wa maji katika Bwawa la Julius Nyerere ilianza kupanda kuanzia tarehe 27 Februari 2026, ambapo kiwango kilikuwa 175.23 masl. Kupanda huku kulichochewa na mvua za wastani hadi juu ya wastani zilizorekodiwa katika vidakio vya Great Ruaha, Kilombero na Luwegu.

- Kasi ya kupanda kwa kina cha maji (184masl) katika bwawa kwa mwaka 2026 imekuwa ya haraka zaidi na kuchukua takribani siku 63 tu ikilinganishwa na mwaka 2025.
- Kufikia tarehe 15 Aprili 2026, ongezeko la maji lilipelekea kuanza kwa upunguzaji wa maji katika bwawa ili kuruhusu kina kupanda taratibu, kulinda miundombinu ya bwawa na kuhakikisha usalama wa wananchi waishio maeneo ya chini ya bwawa dhidi ya hatari ya mafuriko.



Mapendekezo

- Kuendelea na upunguzaji wa maji ili kulinda usalama wa miundombinu ya bwawa.
- Kuhakikisha kiwango cha maji kinabaki ndani ya viwango vya juu vya uzalishaji umeme ili kuendelea uzalishaji wa umeme wa maji kwa ufanisi na matumizi mengine ya maji.
- Kuandaa Mpango wa Usimamizi na Uendeshaji wa Bwawa (Dam Management Plan and Operational Manual) utakaotoa mwongozo wa muda mrefu kuhusu usalama, uzalishaji wa umeme, na usalama wa jamii za chini ya bwawa.